## MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI ROBO YA TATU 2016/2017 ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA NEWALA TAREHE 25/04/2017.

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Chitwanga R. Ndembo | - Diwani Mtunguru | -Mwenyekiti |
| 2. | Ndg. Musa M. Chimae | - Mkurugenzi Mtendaji | -Katibu |
| 3. | Mhe. Swalehe F. Amri | - Diwani Chitekete | -Mjumbe |
| 4. | Mhe. Salehe M. Kamtwanje | - Diwani Mpwapwa | -Mjumbe |
| 5. | Mhe. Hashimu B. Namawa | - Diwani M/Mpelepele | -Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mohamed A. Mnyolokoto | - Diwani Muungano | -Mjumbe |
| 7. | Mhe. Shaibu R. Ngumbe | - Diwani Kitangari | -Mjumbe |
| 8. | Mhe. Zaituni L. Nawanda | -Diwani/V/Maalum | -Mjumbe |
| 9. | Mhe. Saidi Y. Mawangwa | - Diwani Makukwe | -Mjumbe |
| 10. | Mhe. Menas M. Likuku | - Diwani Maputi | -Mjumbe |
| 11. | Mhe. Bakari C. Mniyopa | - Diwani Malatu | -Mjumbe |
| 12. | Mhe. Amina Mkanangwamba | - Diwani/V/Maalum | -Mjumbe |
| 13. | Mhe. Sauda R. Rashidi | - Diwani/V/Maalum | -Mjumbe |
| 14. | Mhe. Athumani M. Mniwasa | -Diwani Chiwonga | -Mjumbe |
| 15. | Mhe. Munga Mohamedi | - Diwani Mchemo | -Mjumbe |
| 16. | Mhe. Jamali J. Nandonde | - Diwani Chilangala | -Mjumbe |
| 17. | Mhe. Rashidi B. Songoni | - Diwani Chihangu | -Mjumbe |
| 18. | Mhe. Fabian J. Mahanyuka | - Diwani Mnyambe | -Mjumbe |
| 19. | Mhe. Hanafi N. Nahonyo | - Diwani Mtopwa | -Mjumbe |
| 20. | Mhe. Rashidi H. Lugomba | - Diwani Nakahako | -Mjumbe |
| 21. | Mhe. Raia R. Nang'oko | - Diwani Mikumbi | -Mjumbe |
| 22. | Mhe. Yahaya A. Lisinge | - Diwani Nandwahi | -Mjumbe |
| 23. | Mhe. Rashidi Nambomo | - Diwani Mnyeu | -Mjumbe |
| 24. | Mhe. Selemani M. Hiyari | - Diwani Mkoma II | -Mjumbe |
| 25. | Mhe. Maua Makubui | -Diwani/V/Maalum | -Mjumbe |
| 26. | Mhe. Zainabu R. Mpita | - Diwani/V/Maalum | -Mjumbe |
| 27. | Mhe. Zakina A. Mduma | - Diwani/V/Maalum | -Mjumbe |
| 28. | Mhe. Arabia H. Mkwatile | - Diwani/V/Maalum | -Mjumbe |
| 29. | Mhe. Simon F. Nachingulu | - Diwani Nambali | -Mjumbe |
| 30. | Mhe. Hadija M. Likwembe | - Diwani/V/Maalum | -Mjumbe |
| 31. | Mhe. Selemani A. Mtili | - Diwani Mkwedu | -Mjumbe. |

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Rashidi A. Akbar | - Mbunge | -KwaTaarifa. |

**WATAALAMU WALIYOHUDHURIA.**

1. Ndg. Shakira Ahmadi – Afisa Utumishi (W)
2. Eng. Sylvester A. Balama - Mhandisi Ujenzi (W)
3. Ndg. Innocent Magayane - K/Mweka Hazina (W)
4. Ndg. Benaya Sanane - Mchumi
5. Ndg. Christina Kambuga - Afisa M/Jamii (W)
6. Ndg. Msafiri Ngai - Afisa Ugavi
7. Ndg. Wilson F. Mafumba - Mkaguzi wa Ndani (W)
8. Ndg. Magreth Likonda - Afisa Ardhi,Maliasili na Mazingira (W)
9. Ndg. Kalugendo Majidu - Afisa Elimu Sekondari (W)
10. Ndg. Juma I Malilo - kaimu Mhandisiwa Maji (W)
11. Ndg. Nsajigwa Mwakatika - Kaimu Katibu TSC (W)
12. Ndg. Mahundu Innocent - Afisa Ushirika (W)
13. Ndg. Omary Msuya - Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
14. Ndg. Rogers Muganyizi - Afisa Ardhi (W)
15. Dr. Judith Ringia - Mganga Mkuu (W)
16. Ndg. Benjamini Macha - Kaimu Afisa Usafirishaji
17. Ndg.Yusufu S.Mshamu - Afisa Tarafa Chilangala.
18. Ndg.Jamila Nalinga - Mtendaji Kata Muungano.
19. Ndg.Boke Mwita - Mtendaji Kata M/Mpelepele.
20. Ndg.Frank Ntilla - K/Mratibu wa UKIMWI
21. Ndg.Shada Nankoko - K/Afisa Utamaduni
22. Ndg.Samuli A. Ali - K/Mtendaji Kata Mkwedu
23. Ndg.Mussa Mohamedi - K/Mtendaji Kata Mpwapwa
24. Ndg.Selemani Aibu - Mtendaji Kata Mtunguru
25. Ndg.Musa E. Musoma - K/Afisa Elimu Sekondari
26. Ndg.Batuli Nahoda - Mtendaji Kata Mnyambe
27. Ndg.Victoria Lusana - Afisa Tarafa Kitangari
28. Ndg.Agness Mnipalika - Mtendaji Kata Mchemo
29. Ndg.Rukia M. Abeid - Mtendaji Kata Chitekete
30. Ndg.Omari Lyopoto - Mtendaji Kata Chiwonga
31. Ndg.Saidi Ussi - Mtendaji Kata Mnyeu
32. Ndg.Hamisi J. Saidi - K/Mtendaji Kata Mikumbi
33. Ndg. Alford Mpanda - Afisa Kilimo,Umwagiliaji na Ushirika (W)
34. Ndg.Faraji K. Chiponda - Mtendaji Kata Nambali
35. Ndg.Haulii H. Hamisi - Mtendaji Kata Malatu
36. Ndg.Salumu Hassani - Mtendaji Kata Mtopwa
37. Ndg.Amina Mbelenje - K/Mtendaji Kata Maputi
38. Ndg.Selemani Chivambo -K/Mtendaji Kata Nakahako

39. Ndg. Machacha Abdala - Mtendaji Kata Kitangari
40. Ndg. Halfani Halfani - Mtendaji Kata Nandwahi
41. Ndg.Salumu Gheo - Mtendaji Kata Makukwe.
42. Ndg.Emmanuel Msuya - Afisa Utumishi

**WAGENI WAALIKWA WALIOHUDHURIA**

1. Ndg. Edward L. Mukama - Mkuu wa TAKUKURU (W)
2. SSP Jonam Sande - Mkuu wa GEREZA
3. Ndg. Edwin R. Kazengo - Meneja Makonde
4. Ndg. Omary Hisha - Kaim Mkuu wa Polisi (W)
5. Ndg. Celestin Simon Msinje - Mshauri wa Mgambo (W)
6. Ndg. Shabani N. Fungameza - Kaim Afisa Uhamiaji (W)
7. Ndg. Adam Juma - Mwandishi wa Habari TBC
8. Ndg. Mary Santiwa - Mwandishi Gazeti la Mwananchi
9. Ndg. Mohamed Mwaya - Mwandishi wa Habari AZAM TV

**SEKRETARIETI**

1. Ndg. Rashidi Mabaya - Mwandishi wa vikao.

**MUHTASARI NA. 19/2016/2017: KUFUNGUA MKUTANO:**

Mwenyekiti aliwasalimu Wajumbe na wageni waalikwa na kuwakaribisha katika Mkutano wa Baraza la Madiwani. Alifungua Mkutano saa 4:30 asubuhi.

**MUHTASARI NA. 20/2016/2017: KUTHIBITISHA AGENDA:**

Wajumbe walithibitisha agenda zilizowasilishwa na kuridhia zijadiliwe katika kikao.

**MUHTASARI NA. 21/2016/2017: KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 31/01/2017:**

Wajumbe walipitia Muhtasari kwa umakini ukurasa hadi ukurasa na kufanya marekebisho yafuatayo.

Uk 7.

Muhtasari namba imejirudia hivyo muhtasari na **23/2016/2017** ***isomeke*** Muhtasari na **24/2016/2017.**

Wajumbe waliupokea muhtasari huo na kuridhia uwekwe saini ili uwe kumbukumbu

sahihi ya kikao.

**MUHTASARI NA. 22/2016/2017 - YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 01/11/2016:**

Muhtasari Na 17/2016/2017 – Taarifa za Kamati ya Kudumu

**Agizo**

Vikundi vilivyotumbuiza siku ya sherehe ya Makonde Chinyakala vilipwe fedha zao haraka iwezekanavyo.

***Utekelezaji***

Agizo limezingatiwa, vikundi vimelipwa.

Wajumbe walipokea utekelezaji huo na hapakuwa na majadiliano.

**MUHTASARI NA. 23/2016/2017 - MASWALI YA PAPO KWA PAPO:**

**Swali 1**

Mheshimiwa Diwani Kata ya Chilangala aliuliza swali, Kamati ya Fedha,Utawala na Mipango inapewaje mamlaka ya kufanya majukumu ya Baraza?

Afisa Utumishi (W) alijibu kuwa kwenye Kanuni za Halmashauri Kamati ya Fedha,Utawala na Mipango imepewa majukumu hayo.

**Swali 2**

Mheshimiwa Diwani Kata ya Nakahako aliuliza swali, Je ni lini Halmashauri itaweka umeme hata wa sola katika Zahanati ya Mpalu?

Mkurugenzi Mtendaji (W) alijibu kuwa ni kweli kuna changamoto hiyo na si kwa Zahanati ya Mpalu tu kuna Zahanati nyingine pia,hivyo ofisi imeona tatizo hilo na litafanyiwa kazi.

**Swali 3**

Mheshimiwa Diwani kata ya Mdimba aliuliza je Halmashauri ina mpango gani wa kuwapatia Zahanati kata ya Mdimba?

Mkurugenzi Mtendaji Wilaya alijibu kuwa miradi inayoibuliwa na wananchi ndiyo Halmashauri inayoiunga mkono.

**Swali 4**

Mheshimiwa Diwani kata ya Mkoma II aliuliza kuwa ni lini Halmashauri itapeleka watumishi wa Afya katika Zahanati ya Mkoma ili kupunguza changamoto ya watumishi katika Zahanati hiyo?

Mkurugenzi Mtendaji (W) alijibu kuwa kwa sasa Halmashauri ina changamoto ya watumishi lakini kwa kuwa Serikali imeahidi kuajiri watumishi wapya,hivyo ajira zikitoka Mkoma watapewa kipaombele.

**MUHTASARI NA 24/2016/2017: TAARIFA YA MKURUGENZI MTENDAJI**

Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa yake.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kujadili kama ifuatavyo:

Mjumbe alisema kuwa shule ya sekondari Mikumbi hakuna walimu wa sayansi,na katika kupangiwa walimu wa sayansi Mikumbi sekondari amepangiwa mwalimu mmoja tu kwa nini pasiwekwe uwiano wa mgao ili kuweza kutatua changamoto hiyo?

Mkurugenzi Mtendaji alijibu kuwa mgao wa walimu umepangwa na Wizara moja moja kwa moja kwa kila mwalimu na shule aendayo.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo.

**MUHTASARI NA 25/2016/2017: TAARIFA YA MWENYEKITI.**

Mwenyekiti alisema kuwa taarifa yake haikuwekwa kwa maandishi isipokuwa aliwataka Waheshimiwa Madiwani kujiandaa na nane nane.

**MUHTASARI NA 26/ 2016/2017: TAARIFA ZA KAMATI ZA KUDUMU.**

**KAMATI YA MAADILI.**

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na hakukuwa na majadiliano.

**KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI**

Mwenyekiti wa Kamati ya kudhibiti UKIMWI aliwasilisha taarifa ya kamati yake.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na hakukuwa na majadiliano.

**KAMATI YA ELIMU,AFYA NA MAJI**

Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu,Afya na Maji aliwasilisha taarifa ya kamati yake.

Wajumbe walipokea na kujadili kama ifuatavyo:

Mjumbe alisema kuwa Madiwani walihamasisha wananchi kujiunga na CHF, Je hadi sasa kuna mpango gani wa kuwapatia kadi wanachama wapya?

Mratibu wa CHF alijibu kuwa zoezi lilisimama kutokana na changamoto ya vitendea kazi lakini kwa sasa zoezi la kuwapatia kadi linaendelea.

Mjumbe aliuliza kuna mkakati gani wa kurekebisha bomba la maji lililoharibiwa kipande cha Mnyambe – Chihangu?

Mwenyekiti wa kamati alijibu kuwa kupitia zabuni zilizotangazwa na mamlaka ya Maji Makonde kipande hicho kitafanyiwa marekebisho kwa utatuzi wa haraka. Kwa utatuzi wa muda mrefu Halmashauri kupitia mradi wa maji wa Miyuyu na Mnima,kijiji cha Mnyambe kitanufaika kwa utatuzi wa muda mrefu.

Mjumbe alihoji kuhusu mgao wa Redio Newala FM ukoje?

Mkurugenzi Mtendaji alijibu kuwa suala la mgao wa Redio bado halijatolewa ufafanuzi lakini hadi sasa Redio ipo chini ya Halmashauri ya Wilaya Newala.

**KAMATI YA UCHUMI,UJENZI NA MAZINGIRA**

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi,Ujenzi na Mazingira aliwasilisha taarifa ya kamati yake.

Wajumbe walipokea na kujadili kama ifuatavyo:

Mjumbe alihoji je kamati inafahamu tatizo lililopo kwenye barabara Mnayope – Bahati na Mnolela?

Mwenyekiti wa kamati alijibu kuwa kamati inafahamu tatizo hilo na Kandarasi watakapoanza kuchonga barabara watarekebisha na sehemu hiyo.

Mjumbe alihoji shamba lililopo Navanga ni shamba la nini?

Mwenyekiti alijibu kuwa shamba hilo ni la maafisa Ugani lakini dhumuni kubwa ni shamba la kutolea mfano kwa wakulima.

Mjumbe alishauri kuwa pindi Wakandarasi wanapofika maeneo husika yatakayofanyiwa kazi ni vema pia wakaripoti kwa Waheshimiwa Madiwani.

Mjumbe alishauri kuwa pindi barabara zinapochongwa na mifereji iwe inawekwa karibu karibu ili kupunguza kasi ya maji.

Mjumbe alihoji kutaka kujua mchakato wa Makatibu wa vyama vya msingi upoje?

Mwenyekiti alijibu kuwa makatibu wa vyama vya msingi huchaguliwa na bodi za vyama hivyo.

Mjumbe alishauri kuwa mwaka huu sheria na kanuni zifuatwe ili kuondoa urasimu wakati wa bodi kuajiri makatibu.

**KAMATI YA FEDHA,UTAWALA NA MIPANGO**

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri aliwasilisha taarifa ya Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na hakukuwa na majadiliano.

**MUHTASARI NA 27/2016/2017: KUPITIA MCHORO WA MIPANGO MIJI KITANGARI.**

Afisa Ardhi aliwasilisha taarifa ya mapendekezo ya mchoro wa Mipango Miji Kitangari.

Wajumbe walipokea Mchoro huo na kuridhia.

**MUHTASARI NA 28/2016/2017: KUFUNGA KIKAO.**

**KATIBU WA CCM**

Alishukuru kwa mwaliko aliopewa na pia alishukuru na kupongeza Baraza la Madiwani kwa kuhakikisha Ilani ya chama cha Mapinduzi inatekelezwa.

**MKURUGENZI MTENDAJI**

Aliwapongeza Waheshima Madiwani kwa ushiriki wao katika Mkutano wa Baraza

Aliwaomba Waheshiwa Madiwani kutoa ushirikiano wa kuwapatia nyumba/vyumba vya kuishi walimu wapya ili waweze kuishi vizuri na waweze kufurahia maisha na waweze kufua kazi vizuri.

Kuna fedha zimetolewa katika Miradi katika Kata zetu hivyo aliwaomba Waheshima Madiwani kutoa ushirikiano wa kutosha katika kusimamia miradi hiyo.

Aliwaomba Waheshimiwa Madiwani kutoa ushirikiano wakutosha katika mapokezi ya mbio za Mwenge wa Uhuru tarehe 16/5/2017 katika Wilaya ya Newala.

Aliwaomba Waheshimiwa Madiwani kuweka agenda ya kudumu ya Ulinzi wa Mtoto katika vikao vya kisheria. Makemeo yawe yakutosha na Elimu itolewe kuhusu madhara ya mwanafunzi kupata mimba.

**MWENYEKITI WA HALMASHAURI**

Mwenyekiti alisisitiza kuhusu mapokezi ya Mwenge wa Uhuru na michango ya Mwenge na kusema kuwa kila Mheshimiwa Diwani ahakikishe anachangia mchango wa Mwenge wa Uhuru.

Aliwaagiza watendaji wa Kata kusimamia na kuzuia uzoaji wa Mchanga barabarani

Mwenyekiti alisisitiza kuwa maagizo yanayotolewa yafanyiwe kazi hasa kwa maeneo yaliyopelekwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na miradi hiyo iendane na thamani ya fedha.

Mwisho aliomba kwa mhandisi wa Maji Makonde na Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Newala kuhakikisha yanapatikana mabomba ya maji kwa ajili ya kipande cha Mtongwele ili kuondoa changamoto ya Maji kwa Tarafa ya Chilangala. Mwenyekiti alifunga kikao saa 9 : 20 alasiri.

**"UMETHIBITISHWA"**

| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |
| --- | --- |
| **JINA** CHITWANGA R. NAMBO | **JINA** MUSSA M. CHIMAE |
| **Saini**........................... | **Saini**........................... |

**TAREHE** 31/07/2017